WAJIBU - INSTITUTE OF PUBLIC ACCOUNTABILITY

policy forum



Co-fonded by
the European Union

**ANGALIZO:**

Taasisi ya WAJIBU na Policy Forum zimetumia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2024/25 kuandaa taarifa hii rahisi ili kuwezesha wananchi na wadau wa uwajibikaji kuzielewa ripoti za CAG na kudai uwajibikaji pale unapokosekana. Pia, ripoti hii inategemea ukamilifu na usahihi wa taarifa kutoka ripoti za CAG za mwaka 2024/25.

**WAJIBU & Policy Forum © 2026**

# UTANGULIZI

Ripoti ya Utoaji wa Huduma za Jamii ya mwaka 2024/25 imeandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kwa kushirikiana na Policy Forum kwa lengo la kuchambua hali ya uwajibikaji katika utoaji wa huduma nchini. Ripoti hii imeandaliwa chini ya utekelezaji wa Mradi wa Raia Makini unaofadhiliwa na umoja wa ulaya wenye lengo kuimarisha ushiriki wa wananchi katika masuala ya uwajibikaji, usimamizi wa rasilimali za umma pamoja na ufuatiliaji wa utoaji wa huduma za jamii.

Ripoti hii imeandaliwa kwa lengo la kuchambua matokeo ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi (Performance Audit) kwa mwaka wa fedha 2024/25 ili kubaini hali ya utoaji wa huduma za jamii na maeneo yanayohitaji maboresho.

Uchambuzi huu umejikita katika sekta ya afya, elimu, maji, kilimo na huduma kwa makundi maalum katika mikoa ya Dodoma, Mbeya, Kigoma, Katavi, Shinyanga, Rukwa, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Singida, Tabora, Iringa, Njombe, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Kagera. Kupitia ushahidi uliowasilishwa katika ripoti za ukaguzi na Hotuba za Bajeti za Wizara za kisekta, ripoti hii inaonesha mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizobainika na kupendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha uwekezaji wa umma unaleta matokeo yanayotarajiwa kwa wananchi.

Aidha, uchambuzi wa ripoti umezingatia utekelezaji wa malengo ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kupitia mikataba na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa, ikiwemo Umoja wa Mataifa kupitia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Agenda 2063 ya Umoja wa Afrika, Mkataba wa Haki za Mtoto, Mkataba wa Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Azimio la Abuja kuhusu sekta ya afya pamoja na mikakati ya kimataifa ya usalama wa chakula na huduma za maji safi na salama.

Kwa ujumla, ripoti hii inalenga kuonesha kiwango ambacho halmashauri zimefanikiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo ya kitaifa na kimataifa pamoja na matumizi ya fedha za umma katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Matokeo ya uchambuzi huu yanatarajiwa kusaidia Serikali, halmashauri, asasi za kiraia, vyombo vya habari pamoja na wananchi katika kuimarisha uwajibikaji, usimamizi wa rasilimali za umma na maboresho ya utoaji wa huduma za jamii nchini.



# SEKTA YA AFYA

Sekta ya afya ni miongoni mwa sekta za kimkakati katika utekelezaji wa DIRA 2050 kutokana na mchango wake katika kujenga taifa lenye nguvu kazi yenye afya, tija na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Pia, Tanzania iliendelea kutekeleza Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo (FYDP III) uliomalizika June 2026 ambao unaosisitiza uwekezaji katika rasilimali watu na kuboresha huduma za msingi za jamii ikiwemo afya. Kuanzia tarehe 1 July 2026, Tanzania imeanza utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo (FYDP IV) na DIRA 2050.

Katika ngazi ya kimataifa, Tanzania imeridhia na inaendelea kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 3) yanayolenga kuhakikisha maisha bora na ustawi kwa watu wa rika zote. Aidha, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizosaini Azimio la Abuja la mwaka 2001 linalozitaka nchi za Afrika kutenga angalau asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwa sekta ya afya ili kuboresha huduma za afya, miundombinu, dawa, vifaa tiba pamoja na rasilimali watu.

Vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza sera na mikakati mbalimbali ya kisekta ikiwemo Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Tano (2021/22-2025/26), Mpango wa Kitaifa wa Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na Kijana, pamoja na ajenda ya Huduma za Afya kwa Wote (Universal Health Coverage - UHC) inayolenga kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora za afya bila kupata mzigo mkubwa wa kifedha.


Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali iliongeza bajeti ya sekta ya afya kutoka takribani shilingi trilioni 2.46 mwaka 2023/24 hadi shilingi trilioni 2.54 mwaka 2024/25. Hata hivyo, kwa kuzingatia kwamba bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 ilikuwa shilingi trilioni 46.82, sekta ya afya ilitengewa takribani asilimia 5.4 ya bajeti yote ya Serikali.

Kiwango hiki ni chini ya lengo la asilimia 15 lililowekwa na Azimio la Abuja la mwaka 2001, ambalo linazitaka nchi za Afrika kutenga angalau asilimia 15 ya bajeti zao za taifa kwa sekta ya afya. Kutofikia kiwango hicho kunaweza kuathiri upatikanaji na ubora wa huduma za afya kwa kusababisha uhaba wa rasilimali muhimu, ikiwemo dawa, vifaa tiba, miundombinu na watumishi wa afya. Hali hii pia inaweza kupunguza uwezo wa mfumo wa afya kukidhi mahitaji ya wananchi na kukabiliana kwa ufanisi na changamoto za kiafya.



Aidha, kiwango hiki cha uwekezaji kinaweza kuchelewesha utekelezaji wa Lengo la Tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 3), ambalo linalenga kuhakikisha maisha yenye afya na ustawi kwa watu wa rika zote. Ili kuharakisha kufikiwa kwa SDG 3, kuna umuhimu wa kuendelea kuongeza uwekezaji katika sekta ya afya ili kufikia angalau kiwango kinachopendekezwa na Azimio la Abuja, jambo litakalosaidia kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote.

**Kielelezo Na. 1:**
**Mwenendo wa Miaka Mitatu wa Utengaji wa Bajeti ya Sekta ya Afya**




**Jambo la 1:**
**Upungufu wa Zaidi ya Watumishi 207,644 wa Afya Unavyodhoofisha Utoaji wa Huduma za Afya Nchini**

Serikali imeendelea kufanya uwekezaji katika ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini, lakini kwenye sekta ya afya bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa rasilimali watu. Uchambuzi wa ripoti ya CAG ya Ufanisi wa Huduma za Afya ya Uzazi umebaini hadi mwaka 2024/25 sekta ya afya ilikuwa na mahitaji ya watumishi 379,766 lakini waliopo ni 172,122, na kuacha pengo la watumishi 207,644 sawa na asilimia 54.7 ya mahitaji yote. Changamoto hii imeonekana zaidi katika ngazi za msingi za utoaji huduma ambazo ndizo zinazohudumia wananchi wengi, hususan katika maeneo ya vijijini. Jedwali Na. 1 inaonyesha hali ya upungufu wa watumishi wa afya, katika ngazi za msingi za huduma za afya.

**Jedwali Na. 1:**
**Hali ya upungufu wa watumishi wa Afya katika Ngazi za Msingi za Huduma za Afya.**

| Ngazi ya Huduma | Mahitaji | Waliopo | Asilimia ya Upungufu (%) |
|---|---|---|---|
| Zahanati | **113,633** | **48,242** | **58** |
| Vituo vya Afya | **76,228** | **43,021** | **44** |
| Hospitali za Wilaya | **145,640** | **47,006** | **68** |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa | **16,324** | **13,825** | **15** |
| Hospitali za Taifa/Kanda/ Maalum | **27,941** | **20,028** | **28** |

Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Tabora, Lindi, Mtwara, Kagera na Ruvuma imeendelea kukabiliwa na changamoto kubwa za uhaba wa wakunga, madaktari wa uzazi, wataalamu wa maabara na watumishi wa afya katika vituo vya msingi. Katika vituo 30 vilivyokaguliwa na CAG, uchambuzi umebaini muuguzi au mkunga mmoja alikuwa akihudumia hadi wajawazito 10 katika wodi za uzazi na wajawazito 20 katika huduma za kliniki za wajawazito (ANC) na huduma baada ya kujifungua (PNC). Uwiano huu ulizidi viwango vinavyopendekezwa na Sera ya Uuguzi na Ukunga ya nchi ambayo inapendekeza mkunga 1 kwa mjamzito 1 hivyokuongeza mzigo mkubwa wa kazi kwa watumishi waliopo.

## Athari

1. Vifo kwa wajawazito wakati na baada ya kujifungua vinavyotokana na shinikizo la damu la mimba (eclampsia), kutokwa damu nyingi baada ya kujifungua, uchungu wa muda mrefu na maambukizi ya uzazi wakati wa kujifungua. Uchambuzi wa ripoti ya CAG ya ufanisi wa Huduma za Afya ya Uzazi, Tanzania ilirekodi takribani vifo 1,498 vya wajawazito kwa mwaka, hali inayoonesha bado kuna changamoto kubwa katika ubora na upatikanaji wa huduma za dharura za uzazi. Kwa ujumla, kiwango cha vifo vya uzazi nchini kinakadiriwa kuwa takribani 524 kwa kila vizazi hai 100,000 (Taarifa ya Benki ya Dunia, 2023/24), ambacho kiko mbali na lengo la SDG 3.1 la chini ya 70 kwa 100,000 ifikapo 2030.

2. Kuongeza rufaa kwa wajawazito kutoka vituo vya afya kwenda katika hospitali za wilaya au rufaa na kusababisha wagonjwa kuchelewa kupata huduma kwa wakati. Uchambuzi wa ripoti ya CAG ya ufanisi unaonesha asilimia 85 ya vifo vya uzazi katika hospitali za rufaa za mikoa na asilimia 70 katika hospitali za wilaya unahusisha wagonjwa waliotumwa kwa rufaa kutoka vituo vya ngazi ya chini.

3. Ongezeko la wanawake wa vijijini kujifungulia nyumbani.

4. Uwezekano wa kupungua kwa ufanisi pamoja na ongezeko la makosa ya kitaalamu kunakotokana na uchache wa watumishi katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma za afya.

## Nini Kifanyike

1. Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo maalum wa kutoa posho ya kwa watumishi wa afya wanaofanya kazi katika maeneo ya vijijini na mazingira magumu.

2. Serikali kuja na mpango wa kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya nchini, ikiwa ni pamoja na nyumba za wafanyakazi wa afya hasa wale wa vituo vya afya vya vijijini, vifaa tiba na mafunzo kwa watumishi wa afya.

3. Serikali kuongeza utengaji wa bajeti ya afya kufikia 15% ya bajeti ya serikali Azimio la Abuja. Ongezeko hili litasaidia kupunguza uhaba wa watumishi wa kada ya afya kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo.
4. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutengeneza utaratibu utakao ziwezesha halmashauri na kata kutumia wauguzi na wakunga wa kujitolea. Hii ni pamoja na kutengeneza na kutekeleza muongozo wa kujitolea kulingana na sera ya kujitolea katika sekta ya afya iliyotolewa na Serikali. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara ya Afya zinaweza kutumia uzoefu wa utekelezaji wa mwongozo wa walimu wa kujitolea katika elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya maendeleo ya wananchi Tanzania bara wa 2023.

5. Ili kukabaliana na upungufu wa wakunga wa kitaalamu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, iangalie uwezekano wa kuwatambua wakunga wa jadi na kuwapa elimu ya msingi ya afya ya uzazi kwa mama na mtoto wakati na baaada ya kujifungua. Hii itasaidia kupunguza shinikizo kwa wakunga wakitaalamu katika utoaji wa huduma hii hasa katika maeneo ya vijijini na mazingira magumu.

## Jambo la 2:
## Kutotumika kwa Vifaa Tiba vyenye Thamani ya Shilingi Bilioni 5.17.

Licha ya serikali kuendelea kuwekeza fedha nyingi katika kuboresha huduma za afya nchini, uchambuzi wa Ripoti ya CAG ya Serikali za Mitaa umebaini vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 5.17 havikuwa vinatumika katika halmashauri 28 nchini. Kiwango hiki kimeongezeka kwa shilingi bilioni 1.32 ukilinganisha na shilingi bilioni 3.85 iliyoripotiwa mwaka 2023/24 kwenye Halmashauri 25. Vifaa hivi vilijumuisha mashine za uchunguzi, vifaa vya maabara, vifaa vya huduma za mama na mtoto pamoja na vifaa vya huduma za dharura vilivyolenga kusogeza huduma karibu na wananchi. Tatizo hili limechangiwa na ukosefu wa wataalamu wa kuendesha vifaa husika, kutokamilika kwa majengo yaliyopaswa kufungwa vifaa hivyo, ukosefu wa vitendanishi vya maabara, pamoja na changamoto za miundombinu ya umeme na maji. Baadhi ya Halmashauri zilizoathirika na kutotumika kwa vifaa tiba vilivyokwisha nunuliwa vinaonekana kwenye jedwali Na 2;

**Jedwali Na. 2:**
**Baadhi ya Halmashauri zenye Vifaa Tiba Visivyotumika .**

| Halmashauri | Thamani ya Vifaa Tiba Visivyotumika (Shilingi Milioni) |
|---|---|
| Newala TC | **790.51** |
| Kigoma DC | **657.11** |
| Tanga CC | **332.93** |
| Kigoma Ujiji MC | **255.67** |
| Arusha DC | **221.78** |
| Mlele DC | **159.13** |
| Muleba DC | **124.98** |
| Msalala DC | **116.97** |

## Athari

1. Wananchi kuendelea kukosa huduma muhimu za afya hususani huduma za uchunguzi, maabara na matibabu ya kibingwa kwa sababu vifaa vilivyopaswa kutoa huduma hizo havitumiki.
2. Kuongezeka kwa rufaa na msongamano wa wagonjwa katika hospitali za rufaa kutokana na kutotumika kwa vifaa katika vituo vya chini, hivyo kuongeza gharama kwa wananchi na kuchelewesha upatikanaji wa huduma.

3. Kukosekana kwa thamani ya matumizi ya fedha za umma kutokana na kutotumika kwa vifaa vilivyonunuliwa.

## Nini Kifanyike

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuja na mpango mahsusi wa kujengea uwezo watumishi wa afya waliopo katika matumizi ya vifaa tiba vya kisasa

### Jambo la 3:
### Madai ya Shilingi Bilioni 8.12 kutoka Hospitali za Umma Kukataliwa na Bima ya Afya NHIF

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ni chanzo muhimu cha mapato kwa hospitali za umma nchini. Fedha zinazopatikana kupitia NHIF hutumika kununua dawa, vifaa tiba, vitendanishi vya maabara, kugharamia huduma za wagonjwa na kuendesha shughuli za kila siku za hospitali. Hata hivyo, uchambuzi wa ripoti ya CAG umebaini madai ya hospitali za umma ya Shilingi Bilioni 8.12 yamekataliwa na NHIF.

**Shilingi Bilioni 8.12**

Kiwango hiki kimepungua kwa shilingi bilioni 1.52 ukilinganisha na shilingi bilioni 9.64 mwaka 2023/24. Madai mengi yalikataliwa kutokana na dosari za kiutawala, makosa ya uingizaji taarifa za wagonjwa katika mifumo ya TEHAMA, nyaraka za madai kutokukamilika, kutofuata taratibu za NHIF na udhaifu katika usimamizi wa madai ndani ya hospitali. Baadhi ya Hospitali zenye madai yaliyokataliwa na NHIF ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3:**
**Orodha ya Hospitali za Umma kubwa Zilizokataliwa Madai ya NHIF.**

| Mkoa | Hospitali | Kiasi Kilichodaiwa (Shilingi Milioni) | Madai Yaliyokataliwa (Shilingi Milioni) | % ya Madai Yaliyokataliwa |
|---|---|---|---|---|
| Kagera | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba | 2,730 | 170 | 6.23 |
| Dodoma | Hospitali ya Benjamini Mkapa | 22,140 | 3,020 | 13.64 |
| Katavi | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Katavi | 960 | 150 | 15.63 |
| Mbeya | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Mbeya | 13,420 | 1,210 | 9.02 |
| Mtwara | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Ligula | 1,560 | 90 | 5.77 |
| Shinyanga | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Shinyanga | 1,420 | 110 | 7.75 |
| Singida | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Singida | 1,680 | 120 | 7.14 |
| Rukwa | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Sumbawanga | 990 | 90 | 9.09 |
| Tanga | Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Tanga | 2,300 | 120 | 5.22 |

## Athari

1. Kuathiri uwezo wa kifedha wa hospitali husika katika kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi.
2. Wananchi kulazimika kununua dawa au huduma ambazo zingeweza kutolewa ndani ya hospitali hivyo kuongeza gharama za matibabu kwa wananchi.

## Nini Kifanyike

Hospitali kufanya uchambuzi wa mara kwa mara wa sababu za madai kukataliwa na kuchukua hatua za marekebisho. Hii ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha watumishi wanaosababisha hasara zinazoweza kuzuilika kutokana na uzembe katika usimamizi wa madai ya NHIF.

### Jambo la 4:

### Uhaba wa Vituo vya afya, Dawa na Miundombinu Muhimu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Uchambuzi wa ripoti za CAG umebaini pamoja na ongezeko la uwekezaji katika sekta ya afya, bado kuna uhaba wa vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa 30. Uhaba huo upo katika majengo ya hospitali sita za rufaa za mikoa, vyumba vya uangalizi maalum, idara za wagonjwa wa nje na wodi za wagonjwa. Vilevile, kuna uhaba wa vifaa tiba na vitendanishi vya maabara katika hospitali 10 za rufaa za mikoa pamoja na upungufu wa wataalamu wa afya kwenye hospitali 9 za rufaa za mikoa. Baadhi ya dosari kwenye utoaji wa huduma za afya katika hospitali za rufaa za mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaonekana kwenye Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4:**
**Dosari Kwenye Utoaji wa Huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

| Hospitali | Dosari kwenye Utoaji wa Huduma za Afya |
|---|---|
| Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Katavi | • Uhaba wa nafasi ya kuweka vitanda katika majengo ya uangalizi maalumu mfano Wing A Inayoweza kuchukua vitanda 88, imewekewa vitanda 128.<br>• Uhaba wa vitendanishi kwa siku 30 (vitendanishi kwa ajili ya kupima tezi dume, bakteria na kiwango cha damu).<br>• Uhaba wa Wataalamu 6 (daktari wa macho, mfumo wa mkojo, mifupa, upasuaji watoto na kinywa, pua, na koo). |
| Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba | • Uhaba wa vifaa 20 (makabati 4 ya kutunzia vifaa tiba, mashine 4 za huduma za meno, mashine 4 za kurekebisha mfumo wa meno, mashine 1 ya altrasaundi, mashine 1 ya eksirei, mashine ya kuchunguza magonjwa ya ndani bila upasuaji (endoscopy), meza ya upasuaji, viatamizi 4 vya watoto wachanga |
| Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Kigoma | • Uhaba wa vitendanishi kwa siku 240 (vifaa vya kukusanyia damu maabara, na vitendanishi kwa ajili ya kupimia tezi dume, na kifaa cha kupimia kiwango cha mafuta mwilini)<br>• Uhaba wa Wataalamu 24 (daktari 1 wa macho, Mtaalamu 1 wa mionzi, daktari 1 wa ngozi, daktari bingwa 1 wa magonjwa ya viungo vya ndani, daktari bingwa 2 wa upasuaji, daktari 1 wa ganzi, madaktari 6 wa uzazi na wanawake, madaktari wa kawaida 9 namadaktari 2 wa magonjwa ya akili) |
| Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mbeya | • Uhaba wa wataalamu 25 (madaktari 6 wa kawaida, madaktari 2 wa kinywa, madaktari 4 wa mifupa, mtaalamu 1 wa ganzi, daktari 1 wa masikio, pua na koo, daktari 1 wa saratani, daktari 1 wa magonjwa ya damu, daktari 1 wa magonjwa mchanganyiko, daktari 1 wa mfumo wa mkojo, daktari 1 wa meno na wataalamu 6 wa ganzi. |
| Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Moshi | • Kukosekana kwa jengo maalumu la kufulia nguo<br>• Uhaba wa Wataalamu 17 (daktari 1 wa upasuaji, daktari 1 wa huduma za dharura, wataalamu 2 wa ganzi, mtaalamu 1 wa mionzi, daktari 1 wa njia ya mkojo, daktari 1 wa magonjwa mbalimbali, madaktari bingwa 2 wa upasuaji, wataalamu 2 wa mionzi, wataalamu 2 wa magonjwa ya saratani, madaktari 2 wa magonjwa ya akili, madaktari 2 wa magonjwa ya ndani). |
| Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Singida | • Uhaba wa majengo 5 (wodi za wagonjwa wa mifupa na watoto; chumba cha upasuaji mkubwa; na sehemu ya matengenezo ya vifaa tiba na mitambo)<br>• Uhaba wa vifaa 3 (mashine ya MRI, mashine ya kuchuja damu (dialysis), na mashine ya kuchunguza magonjwa ya ndani bila upasuaji (endoscopy).<br>• Uhaba wa Wataalamu 8 (madaktari wa magonjwa ya neva 3, daktari 1 wa magonjwa ya damu, daktari 1 wa magonjwa ya moyo, madaktari 2 wa magonjwa ya saratani, daktari 1 wa magonjwa ya njia ya tumbo). |

| Hospitali | Dosari kwenye Utoaji wa Huduma za Afya |
|---|---|
| **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea** | • Kutokuwapo kwa jengo na vifaa vya watoto wachanga.<br>• Kukosekana kwa vitendanishi vya maabara kwa siku 30.<br>• Uhaba wa Wataalamu 3 (daktari wa magonjwa ya saratani, 1 wa magonjwa ya mfumo wa chakula na 1 wa magonjwa ya neva). |
| **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tabora** | • Uhaba wa majengo ya wodi ulisababisha msongamano mkubwa katika wodi zilizopo.<br>• Kutokuwepo kwa jengo la mazoezi-tiba.<br>• Uhaba wa Vitendanishi kwa ajili ya kupima kinga ya seli nyekundu za damu na vitendanishi kwa ajili ya kupima kiwango cha damu.<br>• Uhaba wa Wataalamu 12 (wataalamu 2 wa ganzi, wataalamu 3 wa magonjwa ya figo, daktari 1 wa mfumo wa mkojo, mtaalamu 1 wa mionzi, madaktari 2 wa meno, daktari 1 wa magonjwa ya ngozi, daktari 1 wa magonjwa ya damu na daktari 1 wa macho). |
| **Hospitali za Mamlaka ya Serikali za Mitaa 17** | Sera ya afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa kila kijiji kiwe na zahanati. Hata hivyo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa 17 kuna upungufu wa zahanati 679 sawa na asilimia 52.31 ya mahitaji halisi katika vijiji 1,411. Kwa sasa kuna zahanati 619 wakati mahitaji halisi ni zahanati 1,298, hali inayosababisha kutotosheleza kwa huduma za afya ngazi ya msingi kwa wananchi. |
| **Hospitali za Mamlaka ya Serikali za Mitaa 18** | Sera ya afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa kila kata kuwe na kituo cha afya. Hata hivyo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa 18 kuna upungufu wa vituo vya afya 248 sawa na asilimia 68.32 ya mahitaji halisi katika kata 376. Kwa sasa kuna vituo vya afya 115 wakati mahitaji halisi ni vituo 363, hali inayosababisha kutotosheleza kwa huduma za afya kwa wananchi. |

## Athari

1. Kukosekana kwa huduma ambazo zingepatikana endapo vifaa tiba vingetumika, hivyo kulazimisha wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya.
2. Kutokuwepo na thamani ya fedha ya vifaa tiba vilivyonunuliwa na kutotumika.
3. Huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani, magonjwa ya moyo, afya ya uzazi, pamoja na huduma za watoto wachanga zinaendelea kuwa adimu katika maeneo mengi ya nchi.

## Nini Kifanyike

1. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ihakikishe ununuzi wa vifaa tiba uendane sambamba na uwepo wa miundombinu ya matumizi ya vifaa hivyo.
2. Wizara ya Afya iongeze ajira na usambazaji wa wataalamu katika vituo vyenye vifaa visivyotumika kutokana na upungufu wa watumishi wenye ujuzi wa kuviendesha na kuvitunza.
3. Halmashauri zihakikishe miundombinu na vitendanishi vinapatikana kabla ya ununuzi wa vifaa vipya.

# SEKTA YA MAJI




Sekta ya maji ina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa kutokana na umuhimu wake katika afya, elimu, uzalishaji, mazingira pamoja na ustawi wa jamii kwa ujumla. Tanzania kupitia DIRA 2050 na Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo (FYDP IV) vinaweka msisitizo katika upatikanaji wa maji safi na salama kama msingi wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Katika ngazi ya kimataifa, Tanzania inaendelea kutekeleza Lengo la Sita la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 6), linalolenga kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama pamoja na huduma bora za usafi wa mazingira. Aidha, Agenda 2063 ya Umoja wa Afrika inaweka mkazo katika usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na ujenzi wa miundombinu ya huduma za msingi. Katika ngazi ya kitaifa, utekelezaji wa malengo haya unaongozwa na Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 (National Water Policy - NAWAPO 2002), ambayo inalenga kuhakikisha upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha kwa wananchi wote, kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, na kuongeza ushiriki wa wadau katika utoaji wa huduma za maji.

Katika kutekeleza sera hii, Serikali kupitia Wizara ya Maji, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), pamoja na mamlaka nyingine za maji, imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji vijijini na mijini kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi. Vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazochangia kupungua kwa vyanzo vya maji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za maji. Jitihada hizi zinaonesha dhamira ya Tanzania ya kuoanisha sera na mipango yake ya maendeleo na malengo ya kimataifa na kikanda ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama, kuboresha afya na ustawi wa wananchi, na kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

kwa mwaka wa fedha 2024/25, sekta ya maji ilitengewa takribani shilingi bilioni 641.88 ikilinganishwa na shilingi bilioni 766.2 mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.2.

**Kielelezo Na. 2:**
Mwenendo wa Miaka Mitatu wa Utengaji wa Bajeti ya Sekta ya Maji



Kupungua huku kwa bajeti kunaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maji, hususan katika maeneo ya vijijini, kwa kuchelewesha ujenzi wa miundombinu na kupunguza upatikanaji wa maji safi na salama. Hali hii inaweza kuongeza matumizi ya vyanzo vya maji visivyo salama na hivyo kuongeza magonjwa yanayotokana na maji machafu. Aidha, kupungua kwa uwekezaji kunaweza kuchelewesha kufikiwa kwa SDG 6 inayohusu upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira, pamoja na kuathiri SDG 3 (afya njema), SDG 4 (elimu bora), na SDG 5 (usawa wa kijinsia). Changamoto hii ni kubwa kutokana na athari zake kwa afya, mahudhurio ya shule na kuongeza mzigo wa kutafuta maji unaowakabili wanawake na watoto.




## Jambo la 1:

### Upungufu wa Maji kwa Wananchi

#### (a) Changamoto katika uzalishaji wa Maji

CAG amebainisha kuwepo kwa upungufu wa maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira (WSSAs) pamoja na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs), hali inayoathiri moja kwa moja upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. Ukaguzi umeonesha kuwa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira 22 zilikuwa na uwezo wa kuzalisha maji wa mita za ujazo 13,871,414 kwa mwaka dhidi ya mahitaji ya mita za ujazo 62,708,761 kwa mwaka, na kusababisha upungufu wa mita za ujazo 48,837,347 sawa na asilimia 77.88 ya mahitaji yote ya maji katika maeneo hayo. Hii ina maana kuwa mamlaka hizo ziliweza kukidhi takribani asilimia 22 tu ya mahitaji ya wananchi.

Vilevile, Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii 54 vilikuwa na uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 10,651,150 za maji kwa mwaka dhidi ya mahitaji ya mita za ujazo 22,856,468, na hivyo kusababisha upungufu wa mita za ujazo 12,205,318, sawa na asilimia 53.40 ya mahitaji yaliyopo. Kwa ujumla, mahitaji ya maji katika mamlaka na vyombo hivyo yalikuwa mita za ujazo 85,565,229 kwa mwaka, wakati uzalishaji halisi ulikuwa mita za ujazo 24,522,564 pekee. Hali hii ilisababisha upungufu wa mita za ujazo 61,042,666 kwa mwaka, sawa na takribani asilimia 71 ya mahitaji yote ya maji. Takwimu hizi zinaonesha kuwa zaidi ya theluthi mbili ya mahitaji ya maji katika maeneo yaliyokaguliwa hayakufikiwa, jambo linalowaacha wananchi wengi bila huduma ya kutosha ya maji safi na salama kwa matumizi ya nyumbani, taasisi za umma, shughuli za kiuchumi, kilimo na mifugo. Baadhi ya Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ambazo zinaupungufu wa kuzalisha maji ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5:**
**Hali ya Upungufu wa Maji kwenye Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira**

| Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira | Mahitaji kwa Mwaka (m3/Mwaka) | Upungufu kwa Mwaka (m3/Mwaka) | Asilimia ya Upungufu (%) |
|---|---|---|---|
| Handeni Main Trunk | 13,478,055 | 10,955,864 | 81 |
| Tunduma | 7,944,840 | 7,770,229 | 98 |
| Makonde Plateau | 8,443,910 | 6,363,410 | 75 |
| Vwawa/Mlowo | 4,798,290 | 4,317,506 | 90 |
| Mafinga | 3,140,649 | 2,282,757 | 73 |
| Rujewa | 2,881,675 | 2,136,710 | 74 |
| Manyoni | 2,438,018 | 1,677,032 | 69 |
| Chunya | 1,825,000 | 1,621,330 | 89 |
| Kibondo | 2,658,660 | 1,487,010 | 56 |
| Biharamulo | 1,839,600 | 1,293,560 | 70 |

### (b) Changamoto kwenye Usimamizi wa Vituo vya Maji, Vyanzo vya Maji na Mabwawa.

Uchambuzi wa ripoti za CAG ulibainisha kati ya vituo 4,007 vya maji vinavyosimamiwa na Vyombo vya Kutoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs), vituo 516 ambavyo ni sawa na asilimia 13 havikuwa vinafanya kazi. Hali hii imeathiri upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa takribani wananchi 714,921, ambao walitarajiwa kunufaika na miundombinu hiyo ya maji.

Vilevile, CAG amebainisha vyanzo 263 kati ya 545 vya maji, sawa na asilimia 48.1 havijawekewa mipaka rasmi ya hifadhi. Pia, mabwawa 145 yanayomilikiwa na Serikali hayajasajiliwa.

## Athari

1. Wananchi kukosa maji ya kutosha kwa matumizi ya nyumbani, shule, vituo vya afya, mifugo na shughuli ndogo za kiuchumi.
2. Wanawake na watoto hubeba mzigo mkubwa zaidi kwa kutumia muda mrefu kutafuta maji, jambo linalopunguza muda wa elimu, kazi za uzalishaji na malezi.
3. Kuongezeka kwa hatari ya magonjwa ya mlipuko kama kutumia, kipindupindu na magonjwa mengine yanayotokana na kutumia maji yasiyo salama.

## Nini Kifanyike

1. Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji ili kuendana na mahitaji halisi pamoja na kuboresha miundombinu ya kusambaza maji ili uzalishaji uendane na ongezeko la watu.
2. Serikali kupitia RUWASA na mamlaka za maji ifanye tathmini na ukarabati wa haraka wa vituo vya maji visivyofanya kazi kwa kuimarisha mifumo ya matengenezo na usimamizi ili kuhakikisha miundombinu ya maji inafanya kazi kwa uendelevu na wananchi wanapata huduma zinazokusudiwa.

3. Halmashauri kwa kushirikiana na serikali za vijiji kuimarisha ulinzi wa vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka ya hifadhi na kusajili mabwawa yote ya Serikali ili kulinda vyanzo vya maji dhidi ya uvamizi, uchafuzi na shughuli nyingine zinazohatarisha upatikanaji wa maji kwa sasa na siku zijazo.

**Jambo la 2:**

## Kusuasua na Kutelekezwa kwa Miradi ya Maji Yenye Thamani ya Zaidi ya Shilingi Bilioni 616.12

CAG amebainisha ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka Hazina na Mfuko wa Taifa wa Maji pamoja na malimbikizo ya madeni ya wakandarasi yenye thamani ya shilingi bilioni 137.08 kwenye miradi 285 ya maji inayotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Wizara ya Fedha. Madeni haya yamesababisha kusimama au kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 616.12 katika maeneo mbalimbali nchini.

**Shilingi Bilioni 616.12**

Aidha, uchambuzi umebaini miradi tisa ya maji yenye thamani ya shilingi bilioni 10.40 ilitelekezwa na wakandarasi kabla ya kukamilika kwa kipindi cha zaidi ya siku 930, huku baadhi ya miradi ikishindwa kutoa huduma iliyokusudiwa licha ya fedha za umma kuendelea kutumika. Pia CAG amebaini Bwawa la Manga liliporomoka kabla ya kukabidhiwa rasmi na kusababisha hasara ya shilingi bilioni 2.1.

### Athari

1. Wananchi kuendelea kukosa huduma ya maji safi na salama licha ya uwekezaji mkubwa wa Serikali kwenye sekta ya maji.
2. Kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na ucheleweshaji wa utekelezaji na marekebisho ya bei.
3. Kupotea kwa thamani ya fedha za umma kupitia miradi iliyotelekezwa au iliyojengwa chini ya viwango vinavyotakiwa.
4. Kuongezeka kwa utegemezi wa vyanzo vya maji visivyo salama na hivyo kuongeza hatari ya magonjwa ya mlipuko.

### Nini Kifanyike

1. Wizara ya Fedha itoe kipaumbele cha mgawanyo wa fedha zinazopatikana kwa shughuli za miradi ya maji.
2. Wizara ya Maji, RUWASA na Mamlaka za Maji ziimarishe usimamizi wa mikataba baina ya wakandarasi na Serikali pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi kwa wakati. Vilevile wakandarasi wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa mikataba wachukuliwe hatua za kisheria.

**Jambo la 3:**

## Udhaifu wa Usimamizi wa Mapato na Mita za Maji Unadhoofisha Uendelevu wa Huduma za Maji

Uchambuzi wa ripoti za CAG umebainisha sekta ya maji inaendelea kukabiliwa na dosari za usimamizi wa mapato na upimaji wa matumizi ya maji, hali inayodhoofisha uwezo wa Mamlaka za Maji kutoa huduma endelevu kwa wananchi. Uchambuzi umeonesha mamlaka mbalimbali za maji zilikuwa na ankara za maji ambazo hazijakusanywa zenye thamani ya Shilingi bilioni 9.07. Baadhi ya Mamlaka za Maji zenye ankara za maji ambazo hazijakusanywa ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali na: 6

**Jedwali Na. 6:**
**Baadhi ya Mamlaka za Maji zenye Ankara za Maji ambazo Hazijakusanywa.**

| Mamlaka ya Maji | Mkoa | Ankara za Maji Zisizokusanywa (Shilingi Milioni) |
|---|---|---|
| Makonde Plateau | Mtwara | 721.01 |
| Igunga | Tabora | 427.94 |
| Mafinga | Iringa | 212.77 |
| Kilwa Masoko | Lindi | 161.93 |
| Rujewa | Mbeya | 160.66 |
| Manyoni | Singida | 147.29 |
| Kasulu | Kigoma | 142.96 |

Dosari hizi zimechangiwa na udhaifu wa mifumo ya upimaji wa matumizi ya maji. Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya vyombo vya huduma ya maji vilikuwa na upungufu wa takribani mita 6,000 za maji, ikiwemo SIMIKE/ILUKI-Rungwe (Mbeya) yenye upungufu wa mita 2,324, Mbambabay-Nyasa (Ruvuma) mita 1,540, Makilenga-Arumeru (Arusha) mita 934 na Lugawaso (Njombe) mita 789. Aidha, kulikuwa na mita nyingi ambazo hazikuthibitishwa na Wakala wa Vipimo, ikiwemo Ubaruku (Mbeya) mita 1,934 na Bukibu (Kagera) mita 1,217.

Upungufu kwenye ankara zisizokusanywa na ukosefu wa mita sahihi unaonyesha kuwa sehemu kubwa ya mapato yanayotokana na huduma za maji hayakusanywi na kutumika ipasavyo katika kuboresha huduma kwa wananchi.

## Athari

1. Kupungua kwa mapato ya Mamlaka za Maji na uwezo wake wa kugharamia matengenezo na upanuzi wa huduma za maji.
2. Wananchi kutozwa bili zisizo sahihi kutokana na ukosefu wa mita au matumizi ya mita zisizothibitishwa.
3. Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Mamlaka za Maji na kucheleweshwa kwa miradi ya maendeleo.

## Nini Kifanyike

1. Mamlaka za Maji ziandae mpango maalumu wa ukusanyaji wa madeni ili kurejesha mapato yanayopaswa kukusanywa.
2. Mamlaka ya Maji iharakishe matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usomaji wa mita na usimamizi wa mapato ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.



# SEKTA YA ELIMU


Sekta ya elimu ni msingi muhimu katika kujenga taifa lenye watu wenye maarifa, ujuzi na uwezo wa kushindana kiuchumi. Kupitia DIRA 2050 pamoja na Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo (FYDP IV), Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika uwekezaji wa rasilimali watu kupitia elimu bora, jumuishi na yenye usawa.

Katika ngazi ya kimataifa, Tanzania inaendelea kutekeleza Lengo Na. 4 la Malengo Endelevu ya Dunia (SDG 4) linalolenga kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora, jumuishi na yenye usawa kwa wote. Aidha, Tanzania imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) 1989, Agenda ya Afrika ya 2063 pamoja na mikataba mingine inayosisitiza haki ya mtoto kupata elimu bora katika mazingira salama na rafiki.

Vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo, Mpango wa Maendeleo Sekta ya Elimu pamoja na programu mbalimbali za kuboresha miundombinu sekta ya elimu, kuongeza ajira za walimu pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Serikali iliongeza bajeti ya sekta ya elimu kutoka trilioni 5.98 mwaka 2023/24 hadi trilioni 6.16 mwaka 2024/25 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 3 tu kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3.

Hata hivyo, taarifa za uchambuzi huu unaonesha baadhi ya halmashauri bado zinakabiliwa na changamoto kubwa za upungufu wa madarasa, walimu pamoja na vifaa vya kujifunzia.

**Kielelezo Na. 3:**
**Mwenendo wa Miaka Mitatu wa Utengaji wa Bajeti ya Sekta ya Elimu**






Uchambuzi wa ripoti za CAG umebaini Mamlaka ya Serikali za Mitaa 22 zilikuwa na shule za msingi na sekondari zenye miundombinu chakavu ikiwemo madarasa 1948, mabweni 33, nyumba za walimu 816, vyoo 1732 na majengo mengine muhimu ya shule 119. Hali hii inachangiwa na ongezeko kubwa la wanafunzi kufuatia utekelezaji wa sera ya elimu bila ada. ucheleweshaji na kukamilika kwa miradi ya elimu kutokana na ucheleweshaji wa fedha za maendeleo pamoja na usimamizi hafifu wa wakandarasi kama inavyoonekana kwenye Jedwali na 7.

**Jedwali Na. 7:**

**Hali ya Upungufu wa Miundombinu kwa Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mtaa**

| Halmashauri | Dosari Iliyobainika | Thamani ya Mradi (Shmilioni) |
|---|---|---|
| ***Halmashauri zenye Miradi iliyokamilika Lakini Haitumiki kutokana na dosari mbali mbali*** | | |
| H/Jiji Dodoma | Ukosefu wa maji kwenye vyoo na ukosefu wa mabweni ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita | **361.00** |
| H/W Ileje | Ukosefu wa miundombinu saidizi na wataalamu wa kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwenye bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule ya msingi Ipapa. | **128.00** |
| H/W Kwimba | Ukosefu wa maji; gesi ya maabara; vitanda; sinki sita za kunawia mikono kwenye mabweni katika shule ya sekondari Mwabomba; shule ya msingi Kakora na maabara ya shule ya sekondari Kilyaboya. | **84.50** |
| ***Miradi Haijatekelezwa Kutokana na Upungufu wa Bajeti*** | | |
| H/W Ludewa | Halmashauri kutotenga mapato ya ndani kwa miradi ya maendeleo kumesababisha kutokamilika kwa chumba cha TEHAMA shule ya sekondari Ulayasi, darasa katika shule ya sekondari Kilondo na vyumba 3 vya madarasa shule ya msingi Nyamalamba. | **198.79** |

## Athari

1. Kushuka kwa ubora wa elimu katika shule za msingi na sekondari kutokana na msongamano mkubwa wa wanafunzi darasani unaowafanya walimu kushindwa kutoa uangalizi wa karibu kwa wanafunzi.
2. Kupunguza muda wa kujifunza na kuongeza uchovu kwa wanafunzi pamoja na walimu kutokana na baadhi ya shule kutumia mfumo wa zamu za asubuhi na jioni
3. Kuongezeka kwa utoro na baadhi ya wanafunzi kukatisha masomo hususan katika maeneo ya vijijini kutokana na mazingira duni ya kujifunzia.

## Nini Kifanyike

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI iunde tume ya kutathmini hali ya shule za msingi na sekondari nchini ili Serikali itambue hali halisi ya miundombinu ya shule hizo na kuja na mpango maalumu wa kuziboresha.

**Jambo la 2:**

## Upungufu wa Walimu na Walimu wa Elimu Maalum Unaendelea Kuathiri Ujifunzaji wa Wanafunzi

Pamoja na jitihada za serikali kuajiri walimu wapya, shule nyingi za msingi na sekondari bado zinaendelea kukabiliwa na upungufu wa walimu wa masomo ya msingi, sayansi, hisabati pamoja na walimu wa elimu maalum. Uchambuzi umebaini katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa 26, kulikuwa na upungufu wa walimu 13,542 wa shule za msingi, sawa na asilimia 34.9 ya mahitaji halisi ya walimu 38,787.

Aidha, katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa 32, uchambuzi umebaini upungufu wa walimu 4,442 wa shule za sekondari, sawa na asilimia 23.6 ya mahitaji halisi ya walimu 18,851. Vilevile, shule za msingi zenye vitengo vya elimu maalum kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa 8 zilikuwa na wanafunzi 1,577 wenye mahitaji maalum huku zikiwa na upungufu wa walimu 221 kati ya mahitaji ya walimu 304, sawa na asilimia 72.7.

## Athari

1. Kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika baadhi ya masomo hususan ya sayansi katika maeneo ya vijijini.
2. Uwiano mdogo wa mwalimu kwa mwanafunzi unaathiri uwezo wa walimu kutoa uangalizi wa karibu kwa wanafunzi darasani.
3. Uhaba wa walimu wenye utaalamu maalum unawanyima fursa wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kupata elimu jumuishi na huduma stahiki za kujifunza.

## Nini Kifanyike

1. Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo maalum wa kutoa posho (hardship allowance) kwa walimu wanaofanya kazi katika maeneo ya vijijini na mazingira magumu.
2. Halmashauri ziongeze ujenzi wa nyumba za walimu katika shule zilizopo maeneo ya pembezoni.
3. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ihakikishe upangaji wa walimu unazingatia mahitaji halisi ya shule za vijijini na mijini ili kupunguza tofauti za upatikanaji wa walimu.

## Jambo la 3:
## Kasoro katika Utekelezaji wa Bajeti Sekta ya Elimu

Licha ya Serikali kuendelea kuwekeza katika utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo na ujenzi wa miundombinu ya shule, uchambuzi wa ripoti ya CAG umebaini shule za umma zinaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa rasilimali muhimu za kujifunzia kutokana na upungufu wa fedha pamoja na matumizi hafifu ya fedha zinazotolewa. Mwaka 2024/25, sekta ya elimu ilikabiliwa na upungufu wa shilingi bilioni 72.05 kwa ajili ya kugharamia vitabu vya kiada na huduma nyingine muhimu za elimu kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8:**
**Upungufu wa Fedha kwa ajili ya Vitabu vya Kiada na Ruzuku ya Elimu bila Malipo mwaka 2024/25.**

| Jambo | Mahitaji/ Bajeti (Shilingi Bilioni) | Kiasi Kilichotolewa (Shilingi bilioni) | Upungufu (Shilingi bilioni) | Asilimia ya Upungufu (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vitabu vya kiada (Shule za Msingi na Sekondari) | 93.68 | 24.31 | 69.37 | 74 |
| Ruzuku ya elimu bila malipo (Mamlaka za Serikali za Mitaa 9) | 13.46 | 10.78 | 2.68 | 20 |

## Athari

1. Ukosefu wa vitabu vya kiada hupunguza muda wa kujisomea, kufanya mazoezi binafsi na kuelewa masomo kwa kina kwa wanafunzi.
2. Ukosefu wa ruzuku ya elimu bila malipo husababisha wanafunzi kusoma katika miundombinu hafifu inayoathiri ufaulu wao.

## Nini Kifanyike

Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Halmashauri kuimarisha uwezo wa wakuu wa shule, kamati za shule na maafisa elimu katika upangaji na usimamizi wa matumizi ya fedha za ruzuku ya wanafunzi. Mafunzo haya yahusishe maandalizi ya bajeti, usimamizi wa fedha na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya shule. Pia, Mlipaji Mkuu wa serikali katika utoaji wa pesa za ununuzi wa vitabu na ruzuku za elimu bila malipo atoe kama zilivoidhinishwa na bunge ili kufikia malengo ya mpango wa nne wa maendeleo katika sekta ya elimu.

# SEKTA YA KILIMO




Sekta ya kilimo inaendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania kutokana na mchango wake katika ajira, usalama wa chakula, malighafi za viwandani pamoja na mapato ya wananchi wengi wa vijijini. Kupitia DIRA 2050 pamoja na Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo (FYDP IV), Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika kilimo chenye tija, matumizi ya teknolojia pamoja na kuongeza thamani ya mazao.

Katika ngazi ya kimataifa na kikanda, Tanzania inaendelea kutekeleza SDG 2 inayolenga kutokomeza njaa na kuhakikisha usalama wa chakula pamoja na Agenda 2063 ya Umoja wa Afrika inayosisitiza kilimo chenye tija na matumizi ya teknolojia. Aidha, Tanzania ni sehemu ya utekelezaji wa Azimio la Malabo na Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Barani Afrika (CAADP) zinazolenga kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo.

Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Kilimo pamoja na mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa mazao kupitia pembejeo, huduma za ugani, skimu za umwagiliaji pamoja na uhifadhi wa mazao.

Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Serikali iliongeza bajeti ya sekta ya kilimo kutoka trilioni 1.46 mwaka 2023/24 hadi trilioni 1.94 mwaka 2024/25 kwa ajili ya pembejeo, huduma za ugani, skimu za umwagiliaji pamoja na uhifadhi wa mazao kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.4.

**Kielelezo Na. 4:**
**Mwenendo wa Miaka Mitatu wa Utengaji wa Bajeti ya Kilimo**




Hata hivyo, ripoti za CAG zimeonesha kuwa bado kuna changamoto kubwa za ucheleweshaji wa pembejeo, upungufu wa maafisa ugani pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi hivyo kufanya wakulima wengi kuendelea kutumia mbinu za kizamani za kilimo, kushindwa kukabiliana na magonjwa ya mimea na mifugo, na kupunguza tija ya uzalishaji.




**Jambo la 1:**

## Utoaji Hafifu wa Mikopo kwa Wakulima Wadogo

Ripoti ya CAG imebaini Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ulipanga kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.3 kwa wakulima wadogo, lakini hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2024/25 ulitoa Shilingi milioni 407 pekee, sawa na asilimia 4 tu ya lengo. Hii ina maana kuwa zaidi ya asilimia 96 ya fedha zilizotengwa hazikuwafikia walengwa. Uchambuzi pia umebaini kuwepo kwa uratibu hafifu kati ya AGITF na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), hali iliyochangia kuchelewesha utoaji wa mikopo. Serikali ilikuwa imepanga kuunganisha mifumo ya taasisi hizi ili kuboresha upatikanaji wa mikopo, lakini hatua hiyo haikutekelezwa kikamilifu. Changamoto hii ni kubwa kwa kuwa zaidi ya asilimia 65 ya wakulima nchini ni wakulima wadogo wenye uwezo mdogo wa kupata mikopo kutoka taasisi rasmi za fedha. Vilevile kutolewa kwa asilimia 4 pekee ya fedha kunamaanisha kuwa wakulima wengi walikosa fursa ya kupata pembejeo bora, mashine za kilimo na teknolojia za kuongeza uzalishaji.

### Athari

1. Wakulima kuendelea kutumia mbinu za jadi zinazochangia mavuno madogo na tija ndogo.
2. Kuhatarisha usalama wa chakula na kupunguza mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi.
3. Wakulima hushindwa kuwekeza katika umwagiliaji, uvunaji wa maji na mbegu zinazostahimili ukame, hivyo kubaki katika hatari kubwa ya kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.
4. Vijana na wanawake hukumbwa na changamoto kubwa za kupata dhamana za mikopo hivyo kupunguza ushiriki wao katika kilimo cha biashara na kuongeza hatari ya umaskini.

### Nini Kifanyike

1. Serikali inashauriwa kuharakisha mageuzi ya mfumo wa mikopo ya kilimo kwa kuondoa mwingiliano wa majukumu kati ya AGITF na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, na kuhakikisha fedha za mikopo zinatolewa kwa wakati. Pia, ianzishe mfumo wa kidijitali wa kufuatilia utoaji na marejesho ya mikopo na kupanua mifuko ya dhamana ili kuwafikia wakulima wadogo kwa ufanisi zaidi.
2. Benki na taasisi za fedha zinahimizwa kubuni mikopo inayozingatia mzunguko wa shughuli za kilimo badala ya masharti ya kawaida ya kibiashara. Pia tunashauri kupunguza masharti magumu ya dhamana na kutumia vikundi vya wakulima na AMCOS kama dhamana mbadala ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo.

3. Mamlaka ya Serikali za mitaa, ziimarishe huduma za ugani na kuendeleza kanzidata za wakulima ili kuboresha uthibitishaji wa walengwa na utoaji wa huduma za kifedha.


**Jambo la 2:**

## Hasara ya shilingi bilioni 16.76 kutokana na udhaifu wa uhifadhi wa chakula

CAG amebaini Serikali ilipata hasara ya Shilingi bilioni 16.76 kutokana na usimamizi usioridhisha wa hifadhi ya nafaka chini ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Kati ya hasara hiyo, nafaka zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.76 ziliharibika kutokana na kubadilika rangi na kutofaa kwa matumizi katika maghala ya Makambako na Songwe.

Shilingi Bilioni
**16.76**

Aidha, nafaka zenye thamani ya Shilingi bilioni 13 sawa na tani 16,000 zilihifadhiwa kwa zaidi ya miaka mitatu kinyume na taratibu za usimamizi wa akiba ya chakula, hivyo kusababisha kupungua kwa ubora wake na kuongeza hatari ya kuharibika.




### Athari

1. Kuongeza hatari ya upungufu wa chakula na kuathiri kaya maskini pamoja na watoto walio katika hatari ya utapiamlo.

2. Upotevu mkubwa wa rasilimali za Serikali zilizowekezwa katika ununuzi, usafirishaji na uhifadhi wa mazao, hivyo kupunguza ufanisi wa matumizi ya fedha za umma.

### Nini Kifanyike

NFRA iimarishe mzunguko wa nafaka na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa akiba ya chakula ili kufuatilia ubora, kiasi na muda wa uhifadhi, ili kusaidia kupunguza uharibifu wa nafaka na hasara kwa Serikali.

**Jambo la 3:**

## Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Utegemezi Mkubwa wa Kilimo cha Mvua

Mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuathiri sekta ya kilimo nchini kupitia ukame, mvua zisizotabirika, mafuriko na mabadiliko ya misimu ya uzalishaji. Uchambuzi wa ripoti ya CAG umebaini kuwa hali mbaya ya hewa pamoja na ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji vimechangia kushuka kwa uzalishaji wa mbegu na mazao. Licha ya sekta ya kilimo kuchangia asilimia 26.3 ya Pato la Taifa na kuajiri zaidi ya asilimia 61 ya nguvu kazi, zaidi ya asilimia 90 ya eneo linalolimwa nchini bado linategemea mvua za asili. Aidha, Wakala wa Mbegu za Kilimo TARI ulizalisha tani 9,169.5 sawa na asilimia 11 pekee dhidi ya mahitaji ya tani 80,000.

## Athari

Kupungua uzalishaji wa mazao kutokana na ukosefu wa mbegu bora pamoja na kuendelea kutegemea kilimo cha mvua katika maeneo mengi ya nchi, hali inayopunguza tija na kipato cha wakulima na kuathiri usalama wa chakula katika kaya nyingi.

## Nini Kifanyike

1. Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inapaswa kuharakisha ujenzi na upanuzi wa miradi ya umwagiliaji, hususan katika maeneo yanayokabiliwa na ukame wa mara kwa mara. Hatua hii itasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao, kuimarisha usalama wa chakula na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

2. Wizara ya Kilimo, TARI na taasisi nyingine za utafiti ziwekeze zaidi katika uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora zinazostahimili ukame, magonjwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Hii itawawezesha wakulima kuendelea kuzalisha hata katika mazingira yenye changamoto za tabianchi na kuongeza tija ya kilimo.

# HUDUMA KWA MAKUNDI MAALUM



Huduma kwa makundi maalum ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa maendeleo jumuishi yanayolenga kuhakikisha hakuna mwananchi anayeachwa nyuma katika mchakato wa maendeleo. Kupitia DIRA 2050 pamoja na sera mbalimbali za kitaifa, Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika uwezeshaji wa wanawake, vijana pamoja na watu wenye ulemavu.

Katika ngazi ya kimataifa, Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali ikiwemo Mkataba wa Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD), pamoja na African Youth Charter inayosisitiza ushiriki na uwezeshaji wa vijana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na halmashauri zimeendelea kutekeleza mpango wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuyawezesha makundi hayo kiuchumi. Aidha, utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia, Sera ya Maendeleo ya Vijana pamoja na sheria mbalimbali, Serikali imeweka mifumo mbalimbali ya kuwawezesha kiuchumi na kijamii kupitia mikopo, huduma za ustawi wa jamii na mipango ya ulinzi wa kijamii. Hata hivyo, ukaguzi wa CAG wa mwaka 2024/25 umebaini kuwa bado kuna changamoto kubwa katika utekelezaji wa huduma hizi, hali inayosababisha makundi haya kuendelea kukabiliwa na umaskini, ukosefu wa fursa za kiuchumi na upatikanaji hafifu wa huduma za msingi.



**Jambo la 1:**

## Huduma za Ustawi wa Jamii kwa Wazee Bado Zinakabiliwa na Changamoto Kubwa

Tanzania ina idadi inayoongezeka ya wazee wanaohitaji huduma za kijamii kutokana na kuongezeka kwa umri wa kuishi, mabadiliko ya mfumo wa familia na kupungua kwa uwezo wa familia kuwahudumia nyumbani. Hata hivyo, vituo vya Serikali vinavyotoa huduma kwa wazee ni vichache na vina uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji yaliyopo.

Uchambuzi wa ripoti ya ufanisi ya CAG kuhusu, "Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii kwa Wazee" uliofanyika katika makazi 13 ya Serikali, yakiwemo Ipuli (Tabora), Kolandoto (Shinyanga), Kibirizi (Kigoma), Njoro, Nunge, Kilima, Magugu, Nyabange na Misufini, umebaini vituo vingi havikukidhi viwango vya msingi vya huduma kutokana na changamoto zifuatazo:

a. **Miundombinu chakavu:** Majengo mengi yalikuwa na nyufa, paa zinazovuja, vyoo visivyotosheleza na mazingira yasiyo rafiki kwa wazee wenye changamoto za kutembea. Vituo vyote 13 vilikosa baadhi ya huduma muhimu na wataalamu wanaohitajika.

b. **Kukosa vibali rasmi vya makazi:** Kati ya wazee 220 waliokaguliwa, wazee 213 sawa na asilimia 96 hawakuwa na vibali rasmi vya makazi. Aidha, asilimia 86 ya taarifa za uchunguzi wa kijamii hazikuwa na uhakiki wa taarifa muhimu, asilimia 88 hazikuwa na taarifa za afya na asilimia 80 hazikuwa na uthibitisho wa hali halisi ya wazee kabla ya kupokelewa, hali iliyozuia upangaji sahihi wa huduma.

c. **Uhaba wa watoa huduma:** Vituo vyote 13 vilikuwa na upungufu wa wataalamu muhimu kama wataalamu wa lishe, tiba ya viungo, wahasibu, maafisa ugavi na madereva. Kiwango cha watumishi kilikuwa asilimia 34 tu ya mahitaji, huku muuguzi mmoja akihudumia wazee 56.

d. **Uhaba wa rasilimali fedha:** Ingawa Wizara ilitengea Shilingi milioni 820 kwa ukarabati wa vituo vitano, kituo kimoja pekee ndicho kilikarabatiwa kutokana na kutotolewa kwa fedha. Majengo mengi, baadhi yakiwa ya tangu miaka ya 1960, yalikuwa chakavu na kukosa miundombinu muhimu kama sehemu za kupandia kwa watu wenye ulemavu.

e. **Changamoto za lishe:** Baadhi ya vituo havikuwa na mipango maalum ya lishe kwa wazee wenye magonjwa sugu kama kisukari, shinikizo la damu, magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo, jambo lililoongeza hatari ya utapiamlo na kuzorota kwa afya.

f. **Ukosefu wa bima ya afya na vifaa saidizi:** Wazee 72 pekee kati ya 220 walikuwa na bima ya afya. Pia kulikuwa na upungufu wa vifaa saidizi kama magongo, fimbo za kutembelea, vifaa vya kusikia na vya kusaidia uhamaji, hali iliyoongeza utegemezi kwa walezi.

### Athari

1. Kushuka kwa ubora wa maisha ya wazee kutokana na mazingira yasiyokidhi mahitaji yao ya afya, usalama na ustawi.
2. Kuongezeka kwa hatari za kiafya, ikiwemo magonjwa, utapiamlo, majeraha na vifo vinavyoweza kuzuilika.
3. Kuongezeka kwa utegemezi kwa walezi kutokana na uhaba wa vifaa saidizi na watumishi.
4. Baadhi ya wazee wenye mahitaji makubwa kushindwa kupata huduma stahiki kutokana na udhaifu wa mifumo ya utambuzi na usimamizi.

## Nini Kifanyike

1. Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kufanya tathmini ya kiufundi ya vituo vyote vya wazee nchini ili kufahamu mahitaji ya ukarabati, huduma zinazohitajika na gharama zake. Hii itasaidia kujua kiasi cha bajeti kinachohitajika katika kuboresha miundombinu ya vituo vya wazee.
2. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu iandae muongozo rasmi utakaowezesha wawekezaji binafsi/taasisi za dini/ Asasi za Kiraia kuanzisha makazi ya wazee.
3. Serikali iimarishe rasilimali watu na huduma za afya kwa kuajiri wataalamu muhimu, kuhakikisha wazee wote wanapata bima ya afya na kuwapatia vifaa saidizi vinavyohitajika.

**Jambo la 2:**

### Changamoto kwenye Uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu (WYDF).

Mfuko huu bado una umuhimu mkubwa kwa uwezeshaji wa kiuchumi wa makundi maalum, lakini uchambuzi wa ripoti ya CAG 2024/25 unaonesha udhaifu mkubwa wa kiutawala, usimamizi wa fedha, mifumo ya taarifa na urejeshaji wa mikopo. Serikali ilirejesha utoaji wa mikopo Julai 2024 baada ya kusitishwa Aprili 2023 ili kuboresha mfumo; hata hivyo, hadi Juni 2025 mwongozo rasmi wa usimamizi wa mikopo ulikuwa bado haujaidhinishwa, jambo lililosababisha tafsiri na utekelezaji usiofanana baina ya Halmashauri.

Uchambuzi umebaini kuwa halmashauri 72 hazikupeleka Shilingi bilioni 13.88 kwenye mfuko wa WYDF katika mwaka 2024/25, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 10.17 ambazo hazikutolewa na halmashauri 76 mwaka 2023/24. Aidha, baadhi ya halmashauri zilitoa mikopo kabla ya kusaini mikataba halali na vikundi vya wanufaika, kwa mfano Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilihamisha Shilingi bilioni 2.17 kwa vikundi 234 bila mikataba iliyokamilika. Hii inadhoofisha msingi wa kisheria wa madai, kuongeza hatari ya mikopo kutorejeshwa na kufanya ufuatiliaji kuwa mgumu.

## Athari

1. Kupungua kwa fursa za kiuchumi kwa wawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kukosa mitaji ya kuanzisha au kupanua shughuli za kiuchumi, hali inayopunguza uwezo wao wa kujiajiri na kuongeza kipato.
2. Kudhoofika kwa juhudi za kupunguza umaskini kwa kutokutolewa kwa fedha zilizotengwa na usimamizi dhaifu wa mikopo hivyo hupunguza uwezo wa halmashauri kutumia mfuko huu kama chombo cha kukuza uchumi na kupunguza umaskini katika jamii

## Nini Kifanyike

Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI iimarishe usimamizi na ufuatiliaji wa utoaji na marejesho ya mikopo katika halmashauri zote. Hii ijumuishwe na utekelezaji wa mwongozo mmoja wa kitaifa, matumizi ya mikataba halali na mifumo madhubuti ya kufuatilia mikopo ili kupunguza upotevu wa fedha na kuongeza uwajibikaji.

# HITIMISHO

Ripoti hii imeonesha kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuboresha huduma za jamii, bado kuna changamoto nyingi zinazohitaji hatua za haraka ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora, na zinazofikika. Ni muhimu kwa Serikali, Bunge, halmashauri, wadau wa maendeleo, Asasi za Kiraia, vyombo vya habari pamoja na wananchi kuendelea kushirikiana katika kuimarisha uwajibikaji, usimamizi wa fedha za umma pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma nchini Tanzania.

Mwisho, utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii utasaidia kuboresha utoaji wa huduma za jamii, kuongeza uwajibikaji wa taasisi za umma pamoja na kuimarisha ustawi wa wananchi.

**MUHIMU**

- Ili kupata taarifa zaidi kuhusu ripoti za CAG za mwaka 2024/25, tembelea tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) **www.nao.go.tz.**
- Ili kupata taarifa zaidi kuhusu ripoti za uwajibikaji, tembelea tovuti ya WAJIBU **www.wajibu.or.tz**

**Dar es Salaam**
Barabara ya Rose Garden
Mtaa wa Ndovu, Nyumba No.10,
S.L.P 13486, Dar es Salaam.
Simu: +255 736 666 916
info@wajibu.or.tz
www.wajibu.or.tz

**Dodoma**
Usomalini Mtaa wa Makole,
Nyumba No. 03,
S.L.P 2089, Dodoma.
Simu: +255 738 375 212
info@wajibu.or.tz
www.wajibu.or.tz

@Wajibu_institute